WAJIBU WA MADARAKA YA VIONGOZI MBALIMBALI SHULENI

A: **BODI YA SHULE:**

Bodi ya shule ni chombo muhimu ambacho kila shule inapaswa kuwa nacho ili kufanikisha lengo la Elimu ya Sekondari/Chuo nchini. Kwa mujibu wa sheria Na.25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 10 ya mwaka 1995, Bodi ya shule imepewa mamlaka ya kusimamia:

- Uongozi na uendeshaji wa mipango yote ya maendeleo ya shule
- Kusimamia nidhamu ya walimu na wanafunzi
- Kusimamia masuala ya fedha za shule

Maelezo kamili kuhusu Bodi ya shule yametolewa katika vifungu vifuatavyo ambavyo kila Mkuu wa shule anapaswa kuvisoma na kuvizingatia.

1. Kifungu Namba 38 cha sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 kama kilivyorekebishwa na sheria ya Elimu Na.10 ya mwaka 1995.
2. Kanuni ya Bodi za shule ya 1979. (The School Board Regulation 1979).
3. The Education (Admission to Public Schools) Regulation 1982
4. The Education (Duration of the school year) Regulation 1984
5. The Education (Corporal Punishment) Regulation 1979.
6. The Education (Examination in Schools) Regulation 1982

MKOA WA MWANZA IDARA YA ELIMU
UZINDUZI WA BODI MPYA ZA SHULE ZA SEKONDARI NA VYUO VYA UALIMU

- Mkoa unapenda kuwapongeza wale wote ambao wamechaguliwa kuwa wajumbe wa Bodi mbalimbali za shule za sekondari ziwe za Serikali au Binafsi.

- Mkoa unapenda pia kuwapongeza wale wote waliochaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bodi za shule/vyuo.

- Uzinduzi wa Bodi mpya au makabidhiano ya madaraka, unajenga utamaduni mpya wa kupeana madaraka au kubadilishana madaraka.

- Kukubali kwenu kuwa wajumbe wa Bodi, kunawapa changamoto kubwa katika sekta ya elimu.

- Kila mjumbe wa Bodi anatambua kuwa elimu ni urithi usioisha na kwamba elimu ni hazina kubwa isiyoisha.

- Kila mjumbe wa Bodi ahakikishe kuwa wanafunzi wanapewa elimu bora inayoendana na karne ya 21.

- Bodi zitambue kuwa wanafunzi wetu wanaingia katika dunia ya uchumi wa akili na dunia ya mashindano ya akili.

- Wanafunzi waelewe kuwa " it is academic quality that counts and not the quantity of passes".

- Wakati wajumbe wa Bodi wanapozungumza na wanafunzi, wanafunzi waelezwe ukweli kuwa katika dunia ya leo, soko la ajira ya kuajiriwa na mwingine ni finyu sana isipokuwa ajira binafsi.

- Wajumbe wa Bodi wawakumbushe walimu majukumu yao kwa wanafunzi ambayo ni pamoja na:

    - To educate them
    - To inform them
    - To enlighten them, so that they become better equiped students
    - To counsel and guide them as parents of the day for better citizens.

- Wajumbe wa Bodi wawaeleze wazi wazi wanafunzi kuwa walimu wanajitahidi kutoa elimu bora, lakini wakati huo huo wanafunzi waelewe kuwa yapo matatizo mengi katika utoaji wa elimu. Yapo matatizo ya upungufu wa walimu, matatizo ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia, majengo, madawa ya maabara, vitabu, matatizo ya fedha hivyo uvumilivu unahitajika wa hali ya juu sana.

- Wajumbe wa Bodi wawaeleze wazi walimu kuwa "the quality of a nation depends on the quality of its teachers. First rate teachers depends on efficiency".

- Wajumbe wa Bodi walielewe hili jambo lifuatalo kama anavyotukumbusha aliyekuwa Rais wetu Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa kwa kutukumbusha mambo yafuatayo:-

"Since Independence, our country has, through different programmes and strategies, been striving to provide quality education and to make education accessible to all. However, as we are all aware, the performance of our education system has deteriorated in recent years resulting in the reversal of some achievements made in areas such as primary school enrolment and adult literacy. One can not deny that the quality of education has suffered". Anazidi kutuambia kuwa:

a) "The Tanzania Education and Training Policy provides new guidance for our system to ensure our smooth entry into the 21st century",

   We must break away from the excessive reliance on the Government and must substitute that with new partnerships.

   Instead of the Government making all the decisions, we want local people and their elected representatives to have greater authority over what goes on in their schools. Rather than having the Government shoulder a bigger financial burden that it can manage, we would like to improve the schools system by harnessing the contribution of others, including that of parents.

   We want to bring decisions closer to the action centres, to give communities parents to bigger say in how schools are run, to get action taken more quickly, to enable to see how their money is spent, and to enable teachers to take responsibility over the quality of education of the children entrusted to them".

   Kwa ushauri huo juu basi,

Wajumbe wa Bodi wakumbuke mambo haya matatu:

i. Aspect one is for each Board member to realise that our schools/colleges have problems.
ii. Aspect two is for each Board member to think on means and ways of solving the many problems which schools face.

iii. Aspect three is for each Board member to start solving the problems of our schools immediately or else they remain problems perpetually.

Maneno haya yote yanatupa changamoto kubwa katika kusimamia maendeleo ya shule zetu kama wajumbe wa Bodi.

SERA ZETU HUKO TULIKO TOKA NA HUKO TUENDAKO:

- Sera huwa zinabadilika ni vizuri wajumbe wa Bodi wakaenda pamwe na mabadiliko ya sera.
- Watekelezaji wa sera mpya ya Elimu na Mafunzo pamoja na sheria ya Elimu No.25 ya mwaka 1995 ni wajumbe wa Bodi.
- Kuna haja ya wajumbe wa Bodi kufahamu mabadiliko yaliyorekebishwa katika sheria ya Elimu No.25 mwaka 1978.
- Kuna haja pia ya kufahamu uundaji wa Bodi, majukumu ya Bodi na wajibu wa Bodi.
- Wajumbe wa Bodi waelewe pia mwelekeo wa elimu kulingana na marekebisho ya sheria ya Elimu No.25 ya mwaka 1978 pamoja na sera ya Elimu na Mafunzo.
- Ili kuelewa mabadiliko ya sheria ya Elimu No25 ya mwaka 1978, hatuna budi kwenda kwenye sera mpya ya Elimu na Mafunzo. Hili ndilo chimbuko la marekebisho.
- Ili kuelewa sera mpya ya Elimu na mafunzo, lazima turudi nyuma kidogo na kutazama sera zetu za Elimu tangu tupate uhuru:

  - Mwaka 1962: Sera ya kuondoa ubaguzi katika elimu. Kabla ya hapo kulikuwa na shule tofauti za Wazungu, Waasia na Waafrika.
  - Mwaka 1964: Sera ya Tanzania kujitosheleza katika wataalamu wake yenyewe ifikapo mwaka 1980.
  - Mwaka 1967: Sera ya Elimu ya Kujitegemea
  - Mwaka 1970: Sera ya kufuta ujinga wa kutojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, lengo lilikuwa kufuta Ujinga ifikapo mwaka 1975.
  - Mwaka 1974: Sera ya Elimu kwa Watoto wote. (U.P.E).

- Tume ya Makweta ya Mfumo wa Elimu. "The Presidential Commission of Education".

- Mwaka 1990: Mkutano wa Dunia kuhusu Elimu na Hali za Watoto (EFA). Mkutano ulilenga kwenye Elimu ya Watu Wazima na Elimu kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule.

KUZALIWA KWA SERA MPYA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 1995:

- Sera ilianza kubuniwa mwaka 1993
- Sera ilikubaliwa na Serikali mwaka 1995
- Sera ina jumla ya vipengele 149
- Sera itatekelezwa hatua kwa hatua
- Muswada wa kurekebisha sheria ya Elimu No.25 ya mwaka 1978 ilipelekwa Bungeni katika kikao cha mwezi Aprili, 1995.
- Kuna nyaraka za Kamishna wa Elimu ambazo zimeanza kutolewa
- Kanuni mpya zitatolewa, ndipo zitakazoongoka utekelezaji wa sera mpya ya Elimu na Mafunzo.

LENGO LA MAREKEBISHO YA SHERIA NO.25 YA MWAKA 1978:

- Kuziimarisha Kamati za shule za Msingi na Bodi za shule za sekondari na Vyuo.
- Kuzipa Bodi madaraka na majukumu zaidi ya:

  (a) Kusimamia masuala ya uongozi (Dira – circulars etc)
  (b) Kusimamia masuala ya Utawala (Use of Human Resources & Finance)
  (c) Kusimamia mipango ya Maendeleo
  (d) Kusimamia nidhamu
  (e) Kusimamia mapato na matumizi

- Sera ya Elimu na Mafunzo itatekelezwa hatua kwa hatua ili kulinda mafanikio yaliyopatikana katika kupanua, kuboresha na kuimarisha elimu nchini. Serikali inatambua kuwa yapo mawazo miongoni mwa jamii ya eti viwango vya elimu vimeshuka, hivyo elimu ipewe kipaumbele ili kurejesha imani kwa jamii.

- Sera ya Elimu na Mafunzo ndiyo dira itakayotuelekeza kwenye mafanikio ya elimu katika karne ya 21.

- Sera inalenga kwenye kuweka misingi imara ya elimu itakayoiwezesha Tanzania kwenda pamoja na karne ya 21 ya Sayansi na Teknolojia.

- Sera ya Elimu na Mafunzo inawataka wazazi wachangie zaidi gharama za elimu ya watoto wao.

REGULATIONS MUHIMU:

- Ni vizuri wajumbe wa Bodi wakazifahamu regulations zifuatazo:

(a) The National School Board Regulation
(b) The Private School Board Regulation
(c) The Duration of the School Year Regulation
(d) The National Expulusion and Exclusion from School Regulation
(e) The Corporal Punishment Regulation.

BODI ZA SHULE:

1. Wazazi wa Mkoa wa Mwanza wana sifa ya kuthamini elimu.
2. Kutokana na wazazi wa Mwanza kuthamini elimu, mchango wa Mkoa Kitaifa umekuwa mkubwa.
3. Marekebisho ya sheria ya Elimu No.25 ya mwaka 1978 yameondoa ukiritimba (monopoly) wa Serikali katika uendeshaji na usimamizi wa elimu.
4. Wajumbe wa Bodi wajue madaraka yao pamoja na kanuni zinazowapa madaraka hayo.
5. Katika hali ngumu ya uchumi, Bodi zitambue kuwa wazazi wana mchango mkubwa katika kuendesha shule.
6. Bodi zitambue kuwa elimu inayotolewa Tanzania inasemekana au kudhaniwa ni ya kiwango cha chini, suala hili linagusa mioyo ya wazazi, akili za wazazi na viongozi wa serikali pamoja na kwamba hiyo ni dhana potofu, ni jukumu la Bodi kurekebisha mawazo hayo.
7. Bodi ziyatambue matatizo ya elimu katika shule zao na kuyatafutia ufumbuzi.
8. Bodi zitambue kuwa kosa linalofanyika leo katika shule zetu (kielimu) athari zake katika elimu zitaonekana baada ya miaka 15 hadi 20 ijayo.
9. Bodi ndiyo fimbo/mkongojo imara wa kumsaidia Mkuu wa Shule.
10. Bodi ni chombo chenye nguvu za kisheria (Quasi Judicial).
11. Bodi zitumie nguvu za kisheria zilizopewa.
12. Bodi ndiyo mtawala wa shule
13. Bodi za sasa mwelekeo ni kuwa Bodi za Utendaji badala ya Ushauri.
14. Dhamana ya kusimamia shule imepewa Bodi chini ya Sera ya Elimu na Mafunzo.
15. Bodi zielewe kuwa tunakuwa pale tulipokuwa katika miaka ya 70 na 80

siyo tulipo leo.

16. Kiongozi wa Bodi wa miaka 10 ya nyuma siyio kiongozi wa leo, abadilike na awe “flexible”.
17. Bodi ziwe na busara na hekima, heshima inayostahili.
18. bodi zisaidie shule kupata heshima inayostahili.
19. Bodi zisaidie misingi imara – ili karne ya 21 iwe karne ya matumaini.
20. Bodi zitambue kuwa tuko katika kipindi kigumu cha uchumi hivyo Bodi zina kazi kubwa – asiachiwe Mkuu wa shule peke yake.

MWELEKEO WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

1. Kufanya kazi kwa matokeo (Performance Based Management)
2. Utendaji kazi kwa matokeo (Result Oriented Management)
3. Shule, walimu, kuweka malengo yanayopimika. Utendaji wa mafanikio ya uwajibikaji wa Pamoja (Total Quality Management).
4. Ufundishaji kwa matokeo.
5. Ukubwa wa matatizo yanayoikabili shule katika ufundishaji katika utoaji bora wa elimu ujulikane na ufanyiwe kazi.
6. Ukubwa wa tatizo au matatizo ujulikane (magnitude of the problem).
7. Wajumbe na walimu kushughulikia matatizo ili kuleta mafanikio.
8. Bodi kuboresha taaluma ya shule
9. Katika kuboresha taaluma ya shule Bodi na walimu ni watu muhimu sana. Bodi ni nguzo muhimu na walimu ni nguzo muhimu. Wote ni muhimili muhimu.
10. Walimu wetu, pamoja na uchache wao, na pamoja na matatizo yao, waonyeshe kuwa wanao uwezo.
11. Mshikamano wa Bodi, Mkuu wa Shule, Walimu na Wazazi ni kitu muhimu sana.
12. Bodi ziandae shule kuingia katika mtandao wa kompyuta. Hili ni agizo la Wizara.
13. Hakuna mafanikio yasiyokuwa na matatizo. “Let us all face this challenge”.
14. Wazazi wakubali kubadilika, wanafunzi wakubali kubadilika na walimu wakubali kubadilika ili kuleta maendeleo.

NAWATAKIA KAZI NJEMA YENYE USHIRIKIANO

Ramadhani Chambo Chomola
OFISI YA ELIMU MKOA
MKOA WA MWANZA

Imetolewa na Kifungu 38 (1)

AGIZO LA (UANZISHAJI BODI YA SHULE YA TAIFA THE EDUCATION ACT 1978 (NO.25 OF 1978)

1. Agizo hili litajulikana kuwa Agizo la (uanzishaji) Bodi ya shule ya Taifa, 1979 na kufuatwa na kila shule.

2. Maana ya maneno yaliyotumika katika Agizo hili: "Kamishna"au Afisaelimu Kiongozi – ni Kamishna wa Elimu ya Taifa, pamoja na mtu aliyeteuliwa naye kushika madaraka yoyote ya Kamishna kama ilivyoagizwa chini ya Sheria ya Elimu ya 1978. "Mkuu wa shule" – pamoja na Wakuu wa Vyuo vya Ualimu ambapo Bodi za shule zimeanzishwa.
   "Shule za Taifa" au za serikali ni zile ambazo ziko moja kwa moja chini ya Uongozi wa Wizara ya Elimu.

   Bodi za shule – ina maana ya Bodi zilizoanzishwa chini ya Agizo hili na zitakazoshughulikia masuala ya uendeshaji wa shule za Taifa.

3. Panaundwa Bodi ya shule itakayojulikana kama Bodi ya shule ya Taifa au serikali kwa kila shule ya Taifa au serikali.

4. (i) kila Bodi ya shule ya Taifa au serikali itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mjumbe mmoja, mwakilishi wa shirika anzilishi iwapo lipo.
(b) Afisaelimu wa Mkoa, atakayekuwa kama mwakilishi wa Kamishina.
(c) Mkuu wa Shule
(d) Mjumbe mmoja anayewakilisha walimu
(e) Wajumbe wasiozidi wanne wa kuteuliwa na Waziri/Mkuu wa Mkoa
(f) Wajumbe watatu wa kuteuliwa na Afisaelimu wa Mkoa na kuthibitishwa na Mkuu wa Mkoa.
(g) Wajumbe wawili wa kushirikishwa, watakaochaguliwa na wajumbe wa Bodi na kuthibitishwa na Waziri/Mkuu wa Mkoa.

5. (1) (a) Mwenyekiti wa Bodi atachaguliwa na Wajumbe wa Bodi hiyo, na atatoka kati ya wajumbe hao.
   (b) Afisaelimu wa mkoa au Mjumbe anayewakilisha Walimu hawezi kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti.
   (2) Mwenyekiti atasimamia mikutano yote ya Bodi.
   (3) Endapo Mwenyekiti hatahudhuria mkutano, wajumbe wa Bodi waliopo kwenye mkutano huo, watamchagua Mwenyekiti wa muda kuendesha mkutano huo.

6. (1) Mjumbe wa Bodi, isipokuwa akiacha kuwa mjumbe ataendelea na wadhifa huo kwa kipindi cha miaka minne na mwisho wa kipindi hicho anaweza kuteuliwa au kushirikishwa (co-opted).

(2) Mjumbe wa Bodi ataacha kuwa Mjumbe endapo:-

(a) Atajiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mamlaka iliyomteua au kumshirikisha.
(b) Ushirikishwaji au kuteuliwa kwake kumefutwa na mamlaka iliyomshirikisha au mteua.

(3) Endapo kutatokea nafasi wazi katika ujumbe wa Bodi kutokana na kifo, kujiuzulu au kutomudu kazi (permanent incapacity) kwa Mjumbe yeyote wa Bodi hiyo, mamlaka ya uteuzi itakuwa na uwezo wa kumteua mjumbe mwingine ili kujaza nafasi hiyo, na mjumbe huyo atashika wadhifa huo uliosalia katika kipindi hicho cha miaka minne na mwisho wa kipindi ataweza kuchaguliwa au kushirikishwa kwa kipindi kijacho.

7. (1) Bodi ya shule itakuwa na mikutano yake ya kawaida mara mbili kwa mwaka wakati na mahali pale patakapochaguliwa na Bodi. Bodi itakuwa na uwezo wa kukutana hata zaidi ya mara mbili endapo umuhimu huo utatokea.

(2) Mkuu wa shule atakuwa mwandishi wa Bodi.
(3) Mwandishi kwa kushauriwa na Mwenyekiti, atakuwa na jukumu la kutoa taarifa kuhusu mahali, tarehe, na saa ya mkutano kwa wajumbe na kuhakikisha kuwa kila mjumbe anapata taarifa hiyo mapema kabla ya mkutano.
(4) Endapo wajumbe sita au zaidi; kwa taarifa kimaandishi na kutiwa sahihi, wataomba kuitisha mkutano maalum, basi mwandishi hana budi kuitisha mkutano huo.
(5) Katika kila kikao cha Bodi, uamuzi wa wajumbe wengi waliohudhuria na kupiga kura utakuwa ndio uamuzi wa Bodi na Mwenyekiti atakuwa na kura za uamuzi licha ya kura yake ya kawaida.
(6) Akidi ya lazima kwa kuendesha shughuli zozote za Bodi ya shule ni lazima iwe nusu ya Idadi ya Wajumbe wa Bodi hiyo.
(7) Utendaji wa Bodi utaendelea hata kama kuna nafasi wazi ya wajumbe wa Bodi.
(8) Bodi ina uwezo wa kumkaribisha mtu yeyote ambaye sio Mjumbe wa Bodi hiyo endapo umuhimu wa kufanya hivyo utatokea, ili mradi mtu huyo hatakuwa na uwezo wa

kupiga kura.

(9) Bodi itawajibika kuweka dondoo za mwendelezo wa mikutano yake na kugawa nakala hizo kwa wajumbe na kwa Kamishna.

(10) Bodi inaweza kuendesha shughuli zake inavyoona inafaa ili mradi isikiuke maelekezo ya Agizo hili.

8. (1) Kila Bodi ya shule, kulingana na maelekezo ya jumla au maalum ya Kamishna itakuwa na uwezo wa kufukuza mwanafunzi kutoka kwenye shule ya Taifa au serikali sawa na Kanuni yoyote juu ya kufukuza au kusimamisha kutoka shule iliyotolewa na Waziri katika sheria ya Elimu ya Taifa, 1978.

(2). Bodi ya shule itakuwa na uwezo wa kushauri na kushiriki katika:

(a) Kufanya mapitio na kutoa mapendekezo kwa Kamishna kuhusu uendeshaji na utawala wa shule ambamo Bodi imeanzishwa.
(b) Kujadili na kuhoji masuala yoyote kwenye upeo wa sera ya elimu katika Tanzania, nakuhusiana na wajibu wa Kamishna juu ya shule, na kutoa mapendekezo kwa Kamishna ya jambo lolote la hayo.
(c) Kumshauri Mkuu wa shule kuhusiana na masuala yahusuyo uendeshaji wa shule siku hadi siku.
(d) Kumshauri Kamishna masuala mbalimbali juu ya jambo lololote lile ambalo liliwasilishwa kwa Bodi na Kamishna.
(e) Kuimarisha Elimu na maisha ya shule
(f) Kuanzisha miradi na mipango ya maendeleo ya shule kwa ujumla na kufanya shughuli zozote katika uwezo wake.

KUINUA UBORA WA ELIMU, WAJIBU, NA MAADILI YA UALIMU:

- Mwalimu aone mbele zaidi kuliko wale anaowafundisha – Mwalimu ni “Professional Student”.
- Mwalimu ajali maendeleo ya wanafunzi anaoafundisha. Ualimu uwe “Full Time Job”.
- Mwalimu atambue kuwa wanafunzi wanao uwezo wa kufanya vizuri sana katika masomo kama wataandaliwa vizuri.
- Mwalimu awe mwepesi na kutambua matatizo ya wanafunzi wake anaowafundisha.
- Mwalimu atumie akili zake ili kuwasaidia wanafunzi anaowafundisha.
- Mwalimu awe na uwezo wa mawazo na matendo
- Mwalimu ahamasishe maendeleo ya wanafunzi wake
- Mwalimu ajenge tabia ya utumishi wakujituma na uaminifu.

- Walimu wapande mbegu njema kwa wanafunzi ili jamii isije ikaifukua ile mbegu bora iliyopandwa.
- Kwa kuwa umeamua kuwa mwalimu, lazima uwe na maadili yanayokubalika na jamii.
- Walimu watambue kuwa liko pengo sana kati ya wazee na vijana wa leo.
- Shule kama shule inafanya nini.
- Walimu wetu wanakaaje. Tuanze na walimu waliopo.
- "Motivation" ianze kwa walimu waliopo.
- Walimu wakazanie matumizi ya lugha ya Kiingereza ndani ya darasa na nje ya darasa ambayo ndiyio inatumika katika utahini kitaifaifa.
- Tatizo la upungufu wa wallimu linafahamika.
- Kuna rai ya walimu kukosa motisha.
- Shule za mchanganyiko mara nyingi hazitoi wasichana wengi kwenda Kidato cha Tano, ukilinganisha na wavulana. Tuwape moyo wasichana wajione kuwa wanauwezo sawa wa kiakili kama wavulana. Wasichana watayarishiwe mazingira ambayo hayatakuwa matatizo kwao.
- Walimu wa kike waliopo shuleni, wawape ushauri Nasaha wanafunzi wa kike waliopo.
- Tabia ya walimu inawaambukiza wanafunzi. Walimu wana "influence" kubwa kwa wanafunzi; walimu wana "shape opinion" ya wanafunzi.
- Walimu watambue kuwa karne ya 21 iko nasi, hivyo tuwaandae vizuri wanafunzi wetu kimaadili, kinidhamu, kitaaluma.
- Walimu watambue kuwa, wote kwa pamoja wana 'shared responsibility'.
- Kila mwalimu ahakikishe kuwa kuna "up-ward swing" katika somo analofundisha.
- Walimu wawe wabunifu katika kufundisha na pia wawe wabunifu katika kutatua yanayowakabili katika ufundishaji wao.
- Kazi na wajibu wa Mwalimu vimewekewa taratibu zake ambazo zimetolewa katika sheria ya "Teacher's Service Commission".
- Sheria ya "Teacher's Service commission" imetoa Kanuni (Regulations) ambazo ndizo mwongozo wa utaratibu katika kazi ya ualimu KIMATENDO NA KIMWENENDO.
- Kiwango cha nidhamu ya mwalimu hupimwa kutokana na jinsi mwalimu anavyofuata au kutofuata kanuni zilizowekwa.
- Katibu Mkuu ni Mamlaka ya Nidhamu. "Disciplinary Authority", hii ni pamoja na Mkuu wa shule na mwelekeo mpya, Bodi pia zitakuwa mamlaka ya nidhamu.
- Kanuni zinataja makosa makubwa kama:

    - Kujiweka katika hali ya kushindwa kufanya kazi kwa matumizi ya vileo (ulevi wa kupindukia) au vidonge.
    - Kupatikana na tabia inayoambatana na tabia mbaya "immoral

conduct” k.m. uasherati, ufisadi na wizi.

- Kuiaibisha au kuathiri kazi ya ualimu.
- Kutumia nafasi ya ualimu katika kuchochea mambo ambayo yanaweza kusababisha:

- utovu wa heshima, ufidhuli, uasi, au kutotii serikali halali ya nchi au Serikali yoyote halali iliyowekwa kisheria.
- Hali ya kutotii sheria au amri zozote zilizowekwa kisheria.
- Kuwa katika hali ya kushindwa kutekeleza au kutimiza wajibu wa kazi kwa kiwango kinachoridhisha ili mradi hali hiyo iwe ni matokeo ya kosa lolote lile ambalo mwalimu amelifanya.
- Mwenendo usioridhisha.
- Mwenendo mchafu
- Kutotii walimu na kazi
- Uvivu wa kazi
- Kukataa uhamisho
- Kupigana walimu kwa walimu, walimu na raia wengine
- Kutukana viongozi
- Ukorofi unaoingiliana na kazi
- Kukataa kufundisha
- Kukataa kuhudhuria kozi
- Utoro kazini
- Kuonyesha sifa za kisomo zisizo sahihi
- Kufungua mitihani
- Kuwapa majibu watahiniwa
- Kuwaruhusu wanafunzi wafanye mtihani kinyume cha utaratibu
- Kubadilishana majibu ya mtihani
- Kuonyesha “Sick Sheet” za bandia
- Kulewa wakati wa saa za kazi
- Kuwanywesha pombe wanafunzi.